# MSANII

Toleo la 08



BARAZA LA SANAA LA TAIFA-BASATA
NATIONAL ARTS COUNCIL

*Jisajili kwa kuandika au scan:*

**https//sanaa.go.tz/**

AMIS

# YALIYOMO

Dawati la Katibu Mtendaji..........................................02

Tahariri ya Mhariri......................................................03

Maadili Nguzo ya Ustawi..........................................07

Uzinduzi wa AMIS......................................................09

Mafunzo ya TAUSI na AMIS.......................................11

Matumizi ya Lugha ya Kiswahili................................13

Mchango wa Sanaa kuelekea Uchaguzi wa 2025.....16

Miss World..................................................................20

Mpango mkakati wa BASATA...................................23

Dkt. Mapana ashinda kwa kishindo..........................25

Sanaa Katika Maisha yetu.........................................27

Sanaa na Ongezeko la Pato la Taifa.........................29

Ujenzi waSanaa Imara...............................................31

**Mfumo wa Wadau wa Sanaa,**
**Jisajili kupitia: https://sanaa.go.tz**

**www.basata.go.tz**

**basata.tanzania**

# DAWATI LA KATIBU MTENDAJI



Ndugu Msomaji,wa Jarida la “Msanii”,

Napenda kutumia fursa hii kuwakaribisha kusoma toleo la nane (08) la jarida letu la Msanii la Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). Jarida la Msanii limebeba dhamira ya kukuza, kuenzi na kuendeleza sanaa zetu za taifa. Toleo hili linaakisi mafanikio, changamoto na muelekeo wa sekte ya sanaa nchini, likiwa jukwaa la wasanii, wadau na wapenzi wa sanaa kupata taarifa muhimu, maoni na maarifa ya kujenga tasnia endelevu.

Katika kipindi hiki, BASATA imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa kuzingatia dira yake ya mpango mkakati ambao unamaliza muda wake. Kupitia mikakati hiyo tumeweka msukumo mkubwa katika maeneo ya uratibu wa shughuli za sanaa, ukuzaji wa ubunifu, uendelezaji wa maadili mema katika sanaa pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa wasanii.

Tunafahamu kuwa sekta ya sanaa ina mpango mkubwa sio tu katika kukuza utamaduni wa taifa vilevile katika uchumi wa mtu mmojammoja na taifa kwa ujumla. Hii ndio sababu tumeanzisha mikakati ya kukuza uchumi wa sanaa kwa kuimarisha ushirikiano kati ya serikali, sekta binafsi na wadau wa kimataifa.

Jarida hili limekusanya makala mahususi kutoka kwa wataalamu, wanazuoni na wasanii wenyewe. Tunaleta mbele yenu taarifa za miradi ya kisanaa inayotekelezwa nchini, mafanikio ya wasanii wetu kimataifa pamoja na tafakuri za maendeleo ya sekta yetu.

Napenda kuwashukuru wasanii wote mnaochangia kukuza utambulisho wa kitanzania kupitia kazi zenu. Vilevile, nawapongeza wanahabari, wahariri na timu nzima ya jarida hili kwa kazi kubwa ya kulipa uhai na kulifanya kuwa chombo cha maana cha mawasiliano kati ya BASATA na wadau wake.

Tukiwa tunaendelea na safari ya mageuzi katika sekta ya sanaa tuendelee kushikamana, kushirikiana na kuwekeza katika vipaji vyetu kwa ustawi wa taifa letu kwa sababu wasanii ni nguzo ya utamaduni wa taifa hivyo tuwape nafasi na msukumo katika kazi zao.

**Dkt. Kedmon Mapana**

**Katibu Mtendaji, BASATA**




## SANAA NI NGUZO YA UCHUMI WA TAIFA: NAFASI YA BASATA KATIKA UCHUMI WA UBUNIFU

Katika karne hii ya ishirini na moja, mataifa duniani yameanza kutambua kuwa ukuaji wa uchumi hauwezi tena kutegemea rasilimali asilia pekee kama vile mafuta, madini, au ardhi, vilevile unahitaji kuchochewa na vipaji, ubunifu, na utamaduni wa wananchi wake. Uchumi wa ubunifu umeibuka kama mhimili muhimu wa maendeleo endelevu, ukichangia si tu ukuaji wa pato la taifa pia kuimarisha usawa, kuunda ajira mpya na kukuza utofauti wa kiutamaduni.


Afrika kwa ujumla inakumbatia kasi hii ya mabadiliko kwa kuwekeza zaidi katika sekta za sanaa, utamaduni, muziki, filamu na teknolojia za Kidijitali. Sekta hizi licha ya kuchangia katika kukuza vipaji vya vijana pia kuimarisha tasnia za ndani na kukuza uchumi wa viwanda vya ubunifu. Mataifa kama Nigeria, Afrika Kusini na Kenya yameonesha mafanikio makubwa katika kukuza tasnia hizi. Nchi yetu ya Tanzania nayo inashika hatua thabiti kuelekea kuwa kituo kikuu cha ubunifu na sanaa katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Katika taifa lenye idadi kubwa ya vijana, sanaa ni chanzo muhimu na endelevu cha ajira, iwe rasmi au isiyo rasmi. Kwa kuanzisha na kuimarisha mifumo madhubuti ya urasimishaji wa kazi za wasanii, BASATA inaendelea kuhakikisha kwamba vijana wanapata fursa halali na endelevu za kujiajiri kupitia vipaji na ubunifu wao. Kupitia programu za mafunzo ya kitaalamu, usajili rasmi wa wasanii pamoja na utoaji wa vibali vya kazi za sanaa, Baraza linahakikisha mazingira bora, salama na ya kisheria kwa wasanii kufanya kazi zao. Hii si tu inaboresha hali ya maisha ya wasanii, pia inaongeza tija, ubora, na ushindani wa kazi za sanaa za Tanzania katika soko la kimataifa.

Katika muktadha huu, Tanzania ikiwa na hazina kubwa ya vipaji vya kisanaa na utamaduni wa kipekee, inajiandaa kuimarisha uchumi wa ubunifu kama nguzo muhimu ya maendeleo endelevu na ujumuishaji wa kijamii. Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) linachukua nafasi ya kipekee kama msimamizi, mlezi na mwezeshaji wa sekta ya sanaa nchini, likiwezesha wabunifu, wasanii na wadau wa utamaduni kukuza vipaji vyao, kuongeza ubunifu na kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa taifa.

Kupitia sera, mipango ya kuendeleza na uanzishaji wa miradi, BASATA linahamasisha matumizi ya teknolojia na ubunifu wa kisanaa ili kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya watanzania, huku likihimiza uhifadhi na maendeleo ya tamaduni za asili kama msingi wa utambulisho na mshikamano wa kitaifa.

Tanzania, ikiwa na urithi mkubwa wa utamaduni na vipaji vya kipekee vya sanaa, ina nafasi nzuri ya kutumia fursa hii kuendeleza uchumi wa ubunifu. Muziki, filamu, sanaa za maonesho, mitindo, sanaa za ufundi na tamaduni zetu zina uwezo mkubwa wa kuwa bidhaa za kiuchumi zinazouzwa si tu ndani ya nchi, pia kwa soko la kimataifa. Licha ya kwamba itasaidia katika kuongeza mapato na kukuza uchumi pia itahimiza ukuaji wa sekta ndogondogo, kuleta uwekezaji mpya na kukuza tasnia za kisanaa zenye mvuto wa kimataifa.



Kwa kuwekeza katika sekta hii, Tanzania inaweza kuunda fursa nyingi za ajira kwa vijana na wanawake, kukuza vipaji vipya na kuimarisha utambulisho wa kitaifa kupitia ushawishi wa sanaa na utamaduni. Hii itachangia kukuza sekta ya utalii kwa kuvutia wageni wanaotaka kupata uzoefu wa moja kwa moja wa tamaduni na vipaji vya kipekee vya Tanzania.



## Utalii wa Kiutamaduni na Sanaa

Utalii wa kiutamaduni ni moja ya fursa kubwa za kukuza uchumi inayochochewa kwa kiasi kikubwa na sanaa na mila za asili. Watalii kutoka sehemu mbalimbali za dunia huvutiwa na tamaduni za kipekee kama vile muziki wa asili, ngoma za jadi, mavazi ya kitamaduni, kazi za mikono na sanaa za maonesho. Kwa mfano, nchini Japan utalii unaozunguka tamaduni za Kijapani kama vile kabuki na ikebana huvutia maelfu ya watalii kila mwaka, na nchini Mexico, sherehe za Dia de los Muertos zinavutia watalii wengi wanaotaka kuhudhuria tamaduni za kale za wahispania na Azteki. Kwa kulinda na kukuza sanaa na tamaduni hizi, BASATA inashiriki moja kwa moja katika kuimarisha sekta ya utalii nchini Tanzania, na hivyo kuongeza mapato ya taifa kupitia kuvutia watalii wa ndani na wa kimataifa wanaotafuta uzoefu wa kipekee wa kitamaduni.



## Utambulisho wa Taifa na Sauti ya Tanzania Duniani

Sanaa ni kioo cha jamii na njia muhimu ya taifa kujieleza, kujitambulisha na kuweka alama yake ya kipekee ya utamaduni katika jukwaa la kimataifa. Kupitia sanaa, taifa linaweza kueleza hadithi zake, thamani zake na ndoto kwa ulimwengu mzima. Filamu za Kitanzania zimeanza kupata heshima na kutambulika katika maonesho makubwa ya filamu Afrika na dunia, huku muziki wa Bongo Fleva ukiwa miongoni mwa sauti zinazosikika katika mabara mbalimbali zikivutia mashabiki wa aina tofauti.

Mitindo ya mavazi ya kitanzania pia imeanza kuibuka katika maonesho ya kimataifa kama vile Africa Fashion Week na Dakar Fashion Week, ikionesha ubunifu wa kipekee wa wasanii wa Tanzania. Kwa mfano, filamu kama “Maangamizi: The Ancient One” imepata sifa kubwa Afrika na kimataifa, huku wasanii kama Nasib Abdul (Diamond Platnumz), Rajabu Abdulkar Ibrahim (Harmonizer) na Ali Salehe Kiba (Ali Kiba) wakijitokeza kama nyota wa muziki wa Afrika Mashariki. BASATA ina jukumu la kuhakikisha mafanikio haya yanadumishwa na kuendelezwa kwa kuweka viwango imara, kulinda haki za wasanii na kuhamasisha ubunifu unaoendana na maadili na utamaduni wa taifa.






## Dira ya BASATA katika Uchumi wa Ubunifu

Katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa miaka mitano (2025/26–2029/30), BASATA inalenga kuunda na kuimarisha mazingira bora ya kisera, kisheria na kiutendaji yanayowezesha ukuaji endelevu wa sekta ya sanaa na ubunifu nchini Tanzania. Baraza linapanga kushirikiana kwa karibu na sekta binafsi, wadau wa ndani na wa kimataifa, ili kuimarisha mtandao wa biashara na masoko kwa wasanii.

Katika kipindi kijacho, BASATA itahakikisha urasimishaji wa kazi za sanaa unafanyika kwa ufanisi, urahisi na uwazi zaidi, hivyo kuongeza usalama wa mali za wasanii. Aidha, kupitia programu za elimu ya biashara na ujasiriamali, wasanii wanatakiwa kupata maarifa na ujuzi wa kutosha wa kuendesha shughuli zao kama biashara za kisasa. Vilevile Baraza litahakikisha haki za wasanii zinahifadhiwa kikamilifu kupitia utekelezaji wa sheria mbalimbali. Pia, BASATA itaimarisha ulinzi wa kazi za ubunifu na kukuza uthabiti wa kiuchumi katika sekta hii yenye mchango mkubwa katika uchumi wa nchi.

Sasa ni wakati muafaka kwa Tanzania kutambua, kuthamini na kuweka sanaa kama nguzo madhubuti ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Sanaa siyo tu njia ya kujieleza pekee na kuendeleza urithi wetu wa kitamaduni, pia ni fursa kubwa ya biashara, chanzo cha ajira bora na endelevu. Hata hivyo, Sanaa ni chombo chenye nguvu cha diplomasia ya kiutamaduni kinachoweza kuimarisha mahusiano ya kimataifa na kuvutia uwekezaji wa kigeni. BASATA, kama chombo cha taifa kinachohusika moja kwa moja na kuendeleza na kusimamia sekta ya sanaa nchini, kinajivunia kuwa mstari wa mbele katika kuunda mazingira rafiki, endelevu na yenye tija kwa ukuaji wa uchumi wa ubunifu nchini Tanzania. Kupitia sera madhubuti, usimamizi bora na ushirikiano imara na wadau mbalimbali ikiwemo serikali, sekta binafsi, mashirika ya kiraia na wasanii wenye vipaji, tuna imani thabiti kuwa sanaa haitakuwa tu sehemu ya maisha yetu ya kila siku pia itakuwa nguzo imara. Hivyo basi, tunategemea iwe chachu ya ukuaji endelevu wa uchumi wa taifa letu ikiwahamasisha vijana na kuendeleza ustawi wa jamii kwa ujumla. Hii itatokana na ushirikiano wa pamoja ambao utawezesha kufanikisha ndoto hii ya kuifanya Tanzania kuwa taifa linalojivunia sanaa na utamaduni wake ulimwenguni.

# MAADILI NGUZO YA USTAWI

Usimamizi wa Maadili Nchini Katika Kazi za Sanaa na Mustakabali wa Taifa

Katika mazingira haya mapya ya sanaa yanayoendeshwa na teknolojia na mabadiliko ya kijamii, wasanii wamepata fursa pana ya kujieleza, kushirikisha hadhira zao, na kushawishi mwelekeo wa jamii. Hata hivyo, uhuru huu mkubwa wa kujieleza unapaswa kwenda sambamba na uwajibikaji wa kijamii. Wasanii hawapaswi kuangalia kazi zao kama burudani tu, bali kama majukwaa ya kuelimisha, kuhamasisha na kuimarisha mshikamano wa kijamii. Maudhui wanayochagua kuwasilisha yana uwezo wa kushawishi maadili, mitazamo na mienendo ya watu, hasa vijana ambao ndio kundi kubwa la watumiaji wa sanaa leo hii.

Kwa msingi huo, nafasi ya maadili katika sanaa haiwezi kupuuzwa. Kazi ya sanaa yenye maadili huakisi utu, heshima, mshikamano na matumaini ya jamii. Sanaa inaweza kuwa chombo cha kutibu majeraha ya kihistoria, kukuza utambulisho wa kitaifa na kuongoza jamii katika njia sahihi ya maendeleo. Kinyume chake, sanaa isiyo zingatia maadili inaweza kusababisha mmomonyoko wa maadili, kuchochea migawanyiko au kupotosha mitazamo ya jamii kuhusu masuala nyeti. Hivyo basi, wasanii wanapaswa kuwa makini na kuwajibika katika kile wanachokibuni wakitambua kuwa kazi zao zina nguvu ya kubadilisha maisha ya watu, aidha kwa njia chanya au hasi.



Ili kuhakikisha kuwa kazi za sanaa nchini Tanzania zinatoa mchango chanya katika maendeleo ya jamii. Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa Sura ya 204 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019, ilitumika kuaandaa Mwongozo wa Uzingatiaji Maadili Katika Kazi za Sanaa mwaka 2023. Mwongozo huu ni nyenzo ya msingi inayolenga kuweka viwango vya pamoja vya maadili kwa wasanii, wadau wa sanaa, na jamii kwa ujumla. Unatoa mwongozo wa kimaadili unaozingatia mila na desturi za kitanzania, huku ukiwa na lengo la kulinda heshima ya binadamu, kukuza uzalendo, kudumisha mshikamano wa kitaifa, na kuzuia maudhui yenye athari mbaya kwa jamii, hasa kwa watoto na vijana.

Kupitia mwongozo huo, BASATA inakusudia siyo tu kuzuia kazi zenye maudhui potofu, pia kuchochea ubunifu unaozingatia Utu na Uadilifu, huku likiwajengea wasanii mazingira bora ya kitaaluma yenye uthamini na heshima katika jamii. Hii ni hatua muhimu katika kuijenga sekta ya sanaa kuwa rasmi, yenye mchango wa moja kwa moja katika maendeleo ya uchumi wa taifa na ustawi wa kijamii.

Kazi ya sanaa yenye ujumbe chanya huamsha fikra, huelimisha, huburudisha na kujenga mshikamano katika jamii. Kwa mantiki hiyo, maadili si kikwazo kwa ubunifu bali ni dira ya msanii kuelekeza kipaji chake kwa manufaa ya jamii na taifa kwa ujumla. Kupitia mwongozo huu, wasanii wanaelekezwa kutambua kuwa kazi zao zinawafikia hadhira mchanganyiko, hivyo zinapaswa kujali uzito na athari ya ujumbe unaowasilishwa.



**Msanii Kama Kioo cha Jamii**

Msanii anapofanya kazi bila kuzingatia maadili huacha doa katika jamii, kwani kazi ya sanaa hufikia makundi mbalimbali ya watu wakiwemo watoto, vijana na watu wazima. Maudhui yanayopotosha huweza kuathiri fikra, mitazamo na mwenendo wa jamii kwa ujumla. Kwa sababu hiyo, msanii ana nafasi nyeti ya kuwa kiungo kati ya ubunifu na maadili ya taifa. Kila kazi anayoiwasilisha kwa jamii inapaswa kuwa na uzito unaolingana na athari zake kwa hadhira.

Lakini msanii anapofuata misingi ya utu, heshima na uadilifu, hubeba dhamana kubwa ya kuelimisha, kuhamasisha, na kubadilisha fikra za wengi kwa njia chanya. Sanaa inayozingatia maadili huleta matumaini, hujenga mshikamano na huinua hadhi ya msanii mwenyewe. BASATA linawahimiza wasanii wote nchini kuwa vinara wa mabadiliko chanya, si tu katika kazi zao, bali pia katika mienendo yao ya kila siku, wakitambua kuwa wao ni kioo cha jamii na mabalozi wa utamaduni wa Kitanzania.

Nafasi ya Kila Mdau Katika Kulinda Maadili ya Sanaa

Maadili si jukumu la msanii pekee. Sekta ya sanaa ni mnyororo wa shughuli unaohusisha watu mbalimbali katika hatua tofauti kuanzia wazo hadi kazi ya mwisho inayofikishwa kwa jamii. Wahusika muhimu kama watunzi wa kazi, wasambazaji, mameneja, DJs, wazalishaji, vyombo vya habari, watumiaji wa mitandao ya kijamii, na hata madereva wa vyombo vya usafiri, wote wana nafasi ya kuhakikisha kazi yoyote ya sanaa inayoifikia hadhira imefuata misingi ya maadili, mila na desturi za mtanzania.

Kwa mantiki hiyo, Mwongozo wa Uzingatiaji Maadili Katika Kazi za Sanaa unaweka bayana wajibu wa kila kundi la mdau. Unasisitiza kuwa kila mhusika anatakiwa kujiridhisha na kazi anayoiandaa, kuisambaza au kuirusha hewani, kabla haijawasilishwa kwa umma. Viongozi wa familia na jamii kwa ujumla nao wana nafasi ya kusimamia maadili katika ngazi ya msingi. Kwa kushirikiana kwa pamoja, tunaweza kujenga sekta ya sanaa yenye weledi, inayoheshimu utu na kuchangia ustawi wa taifa letu kwa njia ya ubunifu wenye maadili. Watanzania wengi, hususan vijana ambao ni kundi kubwa na lenye ushawishi mkubwa katika jamii, wanafuatilia kazi za sanaa kwa ukaribu mkubwa. Sanaa imekuwa sehemu ya maisha ya kila siku kupitia muziki, filamu, maigizo, pamoja na maudhui ya mitandaoni.

Katika mazingira ya sasa ambapo upatikanaji wa maudhui ni rahisi kupitia televisheni, redio, majukwaa ya kidijitali na mitandao ya kijamii kazi za sanaa zisizochujwa zinaweza kuwa chanzo kikuu cha mmomonyoko wa maadili hasa kwa watoto na vijana ambao hujifunza kwa kuona na kusikia. Ni kutokana na changamoto hizo ndipo ulipoibuka umuhimu wa kuwa na Mwongozo wa Uzingatiaji Maadili Katika Kazi za Sanaa, kama dira na kinga ya kulinda misingi ya jamii yetu.

Lengo kuu la mwongozo huu ni kuzuia madhara ya maudhui potofu, kulinda heshima ya taifa, kudumisha utambulisho wa kitanzania, na kukuza kazi za sanaa zenye mchango halisi kwa jamii na uchumi wa nchi. Kupitia mwongozo huo, wasanii na wadau wa sanaa wanahimizwa kuhakikisha kuwa kila kazi wanayowasilisha kwa jamii ina uzito wa kijamii, kiakili, na kimaadili huku ikihamasisha ubunifu chanya unaojenga badala ya kubomoa.



## Majaliwa Azindua Mfumo wa AMIS na Tausi

Katika hatua muhimu inayolenga kuboresha, kuratibu na kuendeleza sekta ya sanaa nchini, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), alizindua rasmi Mfumo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Kazi za Sanaa (AMIS). Uzinduzi huo ulifanyika Aprili 22, 2025, kwenye Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), kilichopo jijini Dar es Salaam. Uzinduzi huu ulifanyika wakati wa kikao kazi cha 15 cha Maafisa Utamaduni na Maafisa Michezo kutoka wilaya na mikoa mbalimbali nchini.

Mfumo wa AMIS, umeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Mfumo huu ni jukwaa la kidijitali linalolosaidia uratibu wa shughuli za sanaa, usajili wa wasanii, ukusanyaji wa mapato na kuweka kanzi data ya wadau wa sanaa nchini. Kupitia mfumo huu, serikali inalenga kusimamia kwa ufanisi zaidi sekta ya sanaa, kuongeza uwazi na kuchochea mapinduzi ya kiuchumi kupitia vipaji vya vijana na wasanii.



Akitoa salaam Katika hafla hiyo, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Hamisi Mwinjuma (Mb), alimaarufu kama MwanaFA, alifafanua kuwa mfumo wa AMIS umeunganishwa na mfumo wa TAUSI kwa usimamizi wa pamoja wa wadau wa sekta hizi. Ufanisi wa mifumo hii umeonekana wazi, ambapo Baraza la Michezo la Taifa (BMT) limeongeza mapato yake kwa zaidi ya asilimia 200. Aliongeza kuwa, mfumo wa AMIS utawezesha wasanii kusajiliwa rasmi, kurasimisha kazi zao na kufaidika moja kwa moja na jitihada za serikali katika kuwalinda kisheria na kuwawezesha kiuchumi. Mfumo huu pia unatoa mwanga mpya kwa sekta isiyo rasmi ya sanaa na burudani, ambayo kwa miaka mingi haikupata nafasi ya kuwa sehemu ya mchakato rasmi wa maendeleo.

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa, Tabia Maulid Mwita pia alihudhuria hafla hiyo, alimpongeza Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa mageuzi makubwa aliyoyafanya kwenye sekta ya Utamaduni na Sanaa visiwani humo. Alisema jitihada hizi ni kiashiria cha dhamira ya viongozi wa serikali zote mbili katika kuhakikisha vipaji vya watanzania vinapewa nafasi ya kuchangia maendeleo ya taifa.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Ndugu. Gerson Msigwa, alisisitiza kuwa kikao kazi cha Maafisa Utamaduni na wale wa Michezo ni sehemu ya utekelezaji wa ajenda za kitaifa katika kuboresha sekta ya utamaduni, sanaa na michezo. Alieleza kuwa, Wizara tayari imefanikisha kuanzishwa kwa vitengo vya sanaa, utamaduni na michezo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwa Maafisa Utamaduni kote nchini.

Katika mahojiano maalum mara baada ya uzinduzi wa mfumo wa AMIS, Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Dkt. Kedmon Mapana, alieleza kuwa uzinduzi wa mfumo huo ni hatua ya kihistoria na mapinduzi makubwa katika usimamizi wa sekta ya sanaa nchini. Alisisitiza kuwa mfumo wa AMIS umeundwa kwa ufanisi mkubwa kwa lengo la kuondoa changamoto za muda mrefu zilizokuwa zinawakabili wasanii, kama vile ukosefu wa takwimu sahihi, usajili usio rasmi na ugumu wa wadau wa sanaa kufikia huduma mbalimbali za serikali. “Kwa mara ya kwanza tuna mfumo wa kidijitali ambao utaunganisha wadau wote wa sanaa, kutoka kwa msanii mmojammoja hadi taasisi kubwa katika jukwaa moja linalorahisisha utendaji, uratibu na ufuatiliaji wa maendeleo ya sekta yetu,” alieleza Dkt. Mapana kwa msisitizo.Katika mahojiano maalum mara baada ya uzinduzi wa mfumo wa AMIS, Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Dkt. Kedmon Mapana, alieleza kuwa uzinduzi wa mfumo huo ni hatua ya kihistoria na mapinduzi makubwa katika usimamizi wa sekta ya sanaa nchini.

Alisisitiza kuwa mfumo wa AMIS umeundwa kwa ufanisi mkubwa kwa lengo la kuondoa changamoto za muda mrefu zilizokuwa zinawakabili wasanii, kama vile ukosefu wa takwimu sahihi, usajili usio rasmi na ugumu wa wadau wa sanaa kufikia huduma mbalimbali za serikali. “Kwa mara ya kwanza tuna mfumo wa kidijitali ambao utaunganisha wadau wote wa sanaa, kutoka kwa msanii mmojammoja hadi taasisi kubwa katika jukwaa moja linalorahisisha utendaji, uratibu na ufuatiliaji wa maendeleo ya sekta yetu,” alieleza Dkt. Mapana kwa msisitizo.

Aidha, alibainisha kuwa mfumo wa AMIS sio tu unatoa nafasi kwa usajili na ufuatiliaji wa kazi za wasanii, pia utawezesha serikali kutambua mchango halisi wa sekta ya sanaa katika pato la taifa. “Kupitia AMIS wasanii wanapata hadhi yao kisheria na kiuchumi. Pia, mfumo utarahisisha kulinda haki za wasanii, kuhakikisha vipaji vinaendelezwa na sekta inakuwa na mchango wa moja kwa moja katika uchumi wa taifa. BASATA tumejipanga kikamilifu kutoa elimu, uhamasishaji na msaada wa kiufundi kwa wasanii wote ili kuhakikisha mfumo huu unawanufaisha kwa kiwango cha juu,” alisema Dkt. Mapana.

Uzinduzi wa mfumo wa AMIS ni ushahidi wa dhahiri wa dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuendeleza na kuinua sekta za sanaa na utamaduni kama nyenzo muhimu ya maendeleo. Kupitia mfumo huu Tanzania inaweka msingi imara wa kuibua, kuendeleza na kulinda vipaji vya wasanii, sambamba na kuhakikisha mchango wao katika uchumi unathaminiwa na kuendelezwa kwa njia endelevu.

Kwa mara nyingine tena, Tanzania inathibitisha kuwa utamaduni si tu kielelezo cha utambulisho wa taifa, bali ni nguvu ya uchumi na maendeleo ya watu wake. Mfumo wa AMIS ni mlango mpya wa fursa kwa wasanii wa kizazi hiki na kijacho.

# MAFUNZO YA TAUSI NA AMIS



## BASATA Yaandika Historia kwa Mafunzo ya AMIS na Tausi Kitaifa

Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) limehitimisha kwa mafanikio makubwa ziara wafanyakazi wake kutoa mafunzo ya kitaifa katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, kwa lengo la kuwawezesha wasanii na maafisa wa serikali kuelewa na kutumia kikamilifu Mfumo wa Anwani ya Msanii (AMIS). Mafunzo haya yameweka msingi imara wa mageuzi ya kidijitali katika sekta ya sanaa kwa kuimarisha ufanisi, ushirikishwaji na usimamizi wa taarifa kwa njia shirikishi na jumuishi.

AMIS na TAUSI, Mifumo Inayozungumza Kwa Lengo Moja

Katika utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhusu uunganishaji wa mifumo ya serikali kwa ajili ya kuongeza tija na kupunguza urudufu wa kazi. BASATA imefanikiwa kuoanisha mfumo wa AMIS na mfumo wa kitaifa wa TAUSI (Takwimu za Usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa), unaosimamiwa na TAMISEMI.

Muunganiko huu wa mifumo unaipa Serikali uwezo wa kutumia takwimu sahihi katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo, huku ukiwapa wasanii huduma stahiki kwa uwazi, haraka na weledi. Hii ni hatua muhimu katika kuleta usawa wa kidijitali na kuhakikisha sekta ya sanaa inakuwa sehemu ya maendeleo jumuishi ya taifa.

Mafunzo ya Kitaifa kwa Mikoa 26 Yenye Dira Moja;

BASATA imefanya mafunzo haya katika mikoa yote ya Tanzania Bara, ikiwaleta pamoja wasanii, maafisa utamaduni, viongozi wa vyama vya sanaa, na maafisa maendeleo ya jamii. Washiriki walijifunza hatua kwa hatua jinsi ya kujisajili katika mfumo wa AMIS, kuhuisha taarifa zao binafsi na za kazi, pamoja na kuelewa umuhimu wa kuwa na anwani rasmi ya msanii kama sehemu ya kurasimisha kazi zao.

Mikoa iliyofikiwa ni pamoja na; - Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Njombe, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida, Songwe, Tabora na Tanga.

Sanaa Yazidi Kupanda Juu kwa Msingi wa TEHAMA

Akizungumzia mafanikio ya mafunzo haya ya kitaifa, Katibu Mtendaji wa BASATA, Dkt. Kedmon Mapana, ambaye ni msomi, msanii na kiongozi mwenye maono makubwa ya mageuzi katika sekta ya sanaa nchini, alisema kwamba, uunganishwaji wa AMIS na TAUSI ni ushahidi tosha wa dhamira ya Serikali katika mageuzi ya kidijitali. Wasanii sasa wanatambulika rasmi, wanapata huduma kwa njia rahisi na wana nafasi kubwa ya kushiriki katika maendeleo ya nchi kwa kutumia takwimu sahihi.

Dkt. Mapana, ambaye anatambulika kwa uongozi wake shirikishi, bunifu na uelewa wa kina kuhusu masuala ya utamaduni na sanaa, ameendelea kuwa chachu ya mabadiliko ya kweli katika sekta hii muhimu. Kupitia dira yake ya kusukuma mbele ajenda ya kisanaa kwa misingi ya utaalamu na teknolojia.



BASATA imejipambanua kuwa taasisi ya kisasa inayoendeshwa kwa weledi na mwelekeo wa kimkakati. Kwa uongozi wa Dkt. Mapana, BASATA imeendelea kuimarisha nafasi ya msanii katika jamii na katika mifumo ya taifa, huku ikiendelea kuhakikisha kuwa kila msanii nchini anapata utambulisho rasmi, fursa za maendeleo, na ushirikishwaji katika mipango ya kitaifa kupitia mifumo ya kidijitali kama AMIS. Pia, anaamini kuwa BASATA itaendelea kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa mfumo huo, kutoa msaada wa kiufundi na kuhakikisha kila msanii nchini anasajiliwa na kupata anwani yake rasmi ya kisanii.

Sanaa ya Tanzania Katika Mwelekeo Mpya

Kupitia mafunzo haya ya kitaifa, BASATA imeonesha dhamira ya dhati ya kujenga sekta ya sanaa inayosimamiwa kitaalamu, kidijitali na kwa kushirikiana na mifumo mingine ya serikali. Hii ni hatua ya msingi katika kuhakikisha kuwa sekta ya sanaa inakuwa nguzo ya uchumi wa taifa inayochochewa na taarifa sahihi, sera bora na mifumo thabiti.

Kwa kutumia AMIS, wasanii wa Tanzania wanapata nafasi ya kuendesha shughuli zao kwa uwazi, ufanisi na heshima, huku wakiungwa mkono na mifumo ya serikali iliyoratibiwa, yakikamilisha dira ya Tanzania ya kidijitali na jumuishi.

Tuchukue Hatua Sasa kwa Mustakabali Bora wa Sanaa Yetu.

Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) linatoa wito maalum kwa wadau wote wa sekta ya sanaa nchini – wakiwemo DJs, MCs, wanamuziki, vikundi vya sanaa za maonesho, wachoraji, wabunifu wa mitindo na wamiliki wa kumbi za burudani na Sanaa kuchangamkia kikamilifu fursa ya usajili kupitia Mfumo wa Anwani ya Msanii (AMIS).

Kwa kupitia mfumo huu wa kisasa:

**a)**Wasanii wanatambulika rasmi na Serikali, jambo linalowarahisisishia kupata vibali, **b)**mikopo, fursa za mafunzo na ushiriki katika miradi ya kitaifa na kimataifa.

**c)**Wamiliki wa kumbi na taasisi binafsi za sanaa wanapata nafasi ya kushirikiana na **d)**Serikali katika kutoa huduma bora kwa kufuata taratibu rasmi na kujipatia hadhi ya kisheria.

**e)**Vikundi vya sanaa na wadau wengine **f)**wanapata jukwaa la kujiimarisha kitaasisi na kushiriki kikamilifu katika ajenda ya maendeleo ya taifa kupitia sanaa.

Tunawaomba wadau wote washiriki kwa vitendo katika kujiandikisha, kuhuisha taarifa zao na kuhamasisha wengine katika jumuiya zao za kisanaa kufanya hivyo. Huu ni wakati wa kufanya sanaa iwe taaluma ya kuheshimika, yenye mchango thabiti katika uchumi wa nchi. Tujitokeze kwa wingi. Tujiunge na AMIS. Tuijenge Sanaa ya Tanzania kwa msingi wa utambulisho rasmi, uwazi na TEHAMA. Kwa usaidizi au maelezo zaidi, tafadhali tembelea www.basata.go.tz au ofisi za BASATA au Kwa Maafisa Utamaduni.

# MATUMIZI YA LUGHA YA KISWAHILI



## Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya: Changamoto na Mchango wake kwa Jamii

Makala inalenga kuchambua kwa muhtasari matokeo ya utafiti wa kitaaluma uliofanywa na Ndugu Adam Hussein Jumbe, aliyewasilisha tasnifu yake kwa ajili ya shahada ya Uzamili ya Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dodoma mwaka 2015. Utafiti huu uliangazia mada yenye kichwa: "Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya: Mifano Kutoka Katika Nyimbo za Mapenzi za Wasanii Inspekta Haroun na Mwanafalsafa (MwanaFA)."

Katika utafiti wake, Jumbe alichambua kwa kina nyimbo kadhaa za mapenzi kutoka kwa wasanii maarufu Inspekta Haroun (jina halisi Haroun Yusuph Mwarabu) na MwanaFA (jina halisi Mheshimiwa Hamis Mwinjuma), kwa lengo la kubaini aina ya lugha inayotumika katika kuwasilisha vionjo vya kimapenzi. Pia, alichunguza sababu zinazowasukuma wasanii kutumia lugha hiyo, pamoja na athari zinazojitokeza kwa hadhira, hususan vijana.

Katika dunia ya leo ambapo vijana ndio kundi kubwa zaidi la watumiaji wa sanaa za maonesho, hususan muziki wa kizazi kipya maarufu kama Bongo Fleva, muziki huu umejipenyeza kwa kasi katika maisha ya kila siku ya watanzania mijini na vijijini. Muziki huu haujabaki kuwa burudani tu, bali umegeuka kuwa jukwaa la mawasiliano ya kijamii, uelekezaji wa mitazamo, hisia na mwelekeo wa kitamaduni.Mojawapo ya sifa kuu inayoibuka katika muziki wa kizazi kipya ni matumizi ya lugha ya kisasa iliyojaa misimu, tashbihi, lugha ya picha na wakati mwingine lugha ya moja kwa moja, ambayo huakisi mazingira halisi ya kijamii na kisaikolojia ya wapenzi wa muziki huo.

Vilevile, makala hii inalenga kuibua mjadala mpana kuhusu nafasi ya lugha katika muziki wa kizazi kipya, changamoto zinazohusiana na matumizi yake, pamoja na fursa zilizopo katika kutumia lugha ya sanaa kwa maendeleo ya kijamii na kitamaduni.

Lugha na Vionjo vya Mapenzi

Katika muziki wa kizazi kipya, lugha imegeuzwa kuwa chombo kinachobeba hisia kali, simulizi binafsi, na taswira halisi za maisha ya kimapenzi. Wasanii hutumia maneno ya moja kwa moja wakati mwingine bila kificho wala kujificha nyuma ya mafumbo ili kuwasilisha kwa uhalisia mapenzi, mahaba, maumivu, shauku na tamaa ya kimapenzi. Utafiti unaonesha kwamba lugha inayotumika mara nyingi ni ile inayogusa hisia moja kwa moja, ikijengwa kwa misingi ya uhalisia wa maisha ya kila siku ya vijana.

Katika nyimbo kama "Mtoto wa Geti Kali" na "Asali wa Moyo" na za Inspekta Haroun, tunaona matumizi makini ya taswira, semi na methali za kisasa, zinazoakisi muktadha wa kijamii wa watumiaji wa muziki huo. Maneno kama "geti kali" si tu yanazungumzia sura au mvuto wa msichana, bali pia yanawakilisha hali ya kijamii ya mvutano kati ya urembo, heshima na mvuto wa kimapenzi. Vilevile, nyimbo kama "Unanitega" ya Mwanafalsafa hujenga mvutano wa kimahaba kwa kutumia lugha ya kejeli na mshawasha wa kihisia.

Matumizi ya misimu, kama vile "kunasa", "kuchizi", "kumwaga asali", au "kubanjuka", huifanya lugha ya muziki huu kuwa hai na ya kisasa, pia huibua mijadala mikali kuhusu nafasi ya maadili na mafunzo ya kijamii katika sanaa. Lugha ya picha hutumika kuonesha mapenzi kama mtego, kama safari, au kama vita ya hisia; na mara nyingine, mapenzi hujengwa kama bidhaa ya soko, ambapo lugha ya soko na ya ujasiriamali huingia kwenye maudhui ya mahaba.



Wasanii hawa wanatumia lugha ya kizazi chao, lugha inayokua na kubadilika haraka mitaani, katika mitandao ya kijamii na midahalo ya vijana. Hali hii hujenga uhusiano wa karibu kati ya msanii na hadhira, na hufanya muziki kuwa si burudani tu, bali pia mawasiliano ya kihisia na kijamii. Vijana wanajitambulisha kupitia lugha hii, wanaitumia kueleza na kueleweka, lakini pia wanaathiriwa nayo kwa namna mbalimbali.

Ingawa lugha hii huonyesha ubunifu mkubwa wa kisanaa, uhalisia wa kihisia na urahisi wa kufikisha ujumbe kwa wasikilizaji, bado huibua changamoto kuhusu mwelekeo wa maadili, nafasi ya mila na desturi, na athari kwa makuzi ya kijana wa kitanzania. Hili linapelekea mjadala mpana, wa je, lugha ya mapenzi katika muziki wa kizazi kipya inasaidia kujenga au kubomoa jamii?

**Sababu za Kuchagua Lugha Hiyo**

Utafiti wa Jumbe unaonesha kwamba matumizi ya lugha yenye hisia kali, misimu, na picha za moja kwa moja katika muziki wa kizazi kipya si jambo la bahati nasibu, bali ni mkakati wa kisanaa na kijamii unaochochewa na sababu mbalimbali muhimu. Miongoni mwa sababu kuu ni; -

**Soko na Hadhi ya Hadhira:** Wasanii wa Bongo Fleva hulenga kuvutia kundi kubwa la vijana, ambao ndio wapenzi wakubwa wa muziki huu. Kwa kutumia lugha nyepesi kueleweka, ya kisasa, yenye mvuto wa kihisia na uhalisia wa maisha ya kila siku, wasanii huweza kuunganika moja kwa moja na wasikilizaji wao. Maneno ya mtaani, misimu inayobadilika kila msimu, na mizunguko ya kihisia huifanya muziki kuwa “wao” – yaani, wa kizazi husika.

**Uhuru wa Kisanaa na Uwasilishaji wa Ukweli:** Wasanii wa kizazi kipya wanajinasibisha na falsafa ya uhuru wa kujieleza. Kwao, muziki ni uwanja wa kusema kile kilicho moyoni, bila kufungwa na maadili ya kale au mila zenye mipaka ya kihisia. Hili huwapa nafasi ya kuchora maisha halisi ya mapenzi;- penzi la kweli, lililojeruhiwa, au lililokosa tumaini. Yote haya yakiwasilishwa kwa lugha iliyojaa maumivu, matumaini au hisia za mvuto wa kimapenzi.

Hisia na Uzoefu Binafsi: Wengi wa wasanii hawa huandika nyimbo zao wakitokea katika mazingira ya uzoefu wa kweli. Mapenzi yaliyosukwa mitaani, yaliyojengwa shuleni, yaliyovunjika kwenye simu au yaliyozaliwa katika muktadha wa umasikini na ndoto zisizotimia. Kwa pamoja husukuma wasanii kutumia lugha ya ndani ya nafsi, yenye nguvu ya kusisimua na kuhamasisha wasikilizaji wao.

Mbinu ya Kusimulia Hadithi: Matumizi ya lugha ya moja kwa moja huwasaidia wasanii kuwasilisha simulizi zao kama hadithi za kweli. Hii huongeza uhalisia, na kusababisha hadhira kuhisi kwamba wimbo huo unazungumza nao moja kwa moja..

# ATHARI KWA JAMII



Matumizi ya lugha katika nyimbo za mapenzi za muziki wa kizazi kipya yana madhara na manufaa yanayochangamana, yakilenga kugusa hisia, kuburudisha, pia kuathiri mienendo ya kijamii, kiutamaduni na kimaadili. Athari hizo zinaweza kugawanywa katika pande mbili ambazo ni faida na mchango chanya kwa jamii.

Kukuza Lugha ya Kiswahili: Nyimbo hizi zinachangia kuongeza msamiati mpya wa Kiswahili, kuhuisha misimu, na kutoa maneno mbadala yanayoakisi mabadiliko ya kijamii. Wasanii huchangia maendeleo ya lugha kwa kuibua misimu mipya, ambayo baadaye inaweza kuingia katika matumizi rasmi, kama ilivyotokea kwa maneno kama “bongo”, “uchakachuaji”, “kuchorwa”, n.k.

Burudani na Upatano wa Hisia: Muziki wa mapenzi hutumika kama tiba ya kihisia kwa wengi. Nyimbo hizi huweza kufariji walioumia, kuhamasisha waliovunjika moyo na hata kudumisha mahusiano kwa kupitia ujumbe unaozungumzia msamaha, matumaini, au upendo wa kweli.

Kuibua Mijadala ya Kijamii: Kwa kushughulikia masuala ya mapenzi waziwazi, nyimbo hizi zinafungua nafasi ya mjadala kuhusu jinsia, mahusiano, uhuru wa kujieleza na maadili mapya ya kizazi kipya.

Madhara na Changamoto Zinazojitokeza:

Mmomonyoko wa Maadili: Lugha wazi kuhusu mapenzi na wakati mwingine ishara zenye maudhui ya ngono vinaweza kuchangia kuporomoka kwa maadili, hususan kwa vijana walio katika umri wa kubalehe. Kuwiana kwa lugha ya picha na mwelekeo wa maadili kunapopotea, jamii hujikuta katika mkanganyiko wa kimaadili.

**Kuhamasisha Mahusiano ya Mapema:**

Kwa kuwa nyimbo nyingi huonesha mapenzi kama jambo la kawaida lisilohitaji ukomavu, vijana wengi hujikuta wakijiingiza katika mahusiano wakiwa bado hawajakomaa kiakili, kijinsia au kijamii. Hili linaweza kusababisha matatizo ya kiafya, kielimu na hata kiuchumi.

**Kudumaa kwa Ubunifu wa Kisanaa:** Katika harakati za kupata umaarufu wa haraka, baadhi ya wasanii huiga mitindo ya lugha kutoka kwa wenzao bila kuongeza thamani mpya ya kisanaa. Hali hii husababisha kurudiarudia maudhui na mtindo, jambo ambalo hudidimiza ubunifu wa kifasihi na kisanaa katika muziki wa kizazi kipya.

**Ufinyu wa Mawazo:** Muziki unapojikita sana katika mapenzi kwa lugha ile ile kila wakati, hupunguza nafasi ya kujadili masuala mengine muhimu ya kijamii kama vile siasa, elimu, afya, au mazingira. Hii ni changamoto kubwa kwa muziki unaotaka kuwa jukwaa la mabadiliko ya jamii.

Utafiti wa Adam Hussein Jumbe unathibitisha kuwa muziki wa kizazi kipya si tu burudani bali pia ni kielelezo cha mabadiliko ya kijamii na kisanaa. Matumizi ya lugha ndani ya muziki huu yanaonyesha mwelekeo wa kijamii na kitamaduni kwa kizazi cha sasa. Ni wajibu wa wadau mbalimbali wakiwemo wazazi, walimu, viongozi wa dini, pamoja na taasisi za kisanii, kushirikiana kuhakikisha muziki huu unakuwa chombo cha kujenga jamii na si kuibomoa.

# MCHANGO WA SANAA KUELEKEA UCHAGUZI WA 2025



## Kulinda Amani, Wasanii Wana Nafasi Katika Uchaguzi Mkuu wa Tanzania 2025

Katika muktadha huu wa kisiasa wenye mabadiliko makubwa, Sanaa inakuwa daraja la kuunganisha wananchi, ikiwahamasisha kushiriki kwa njia ya amani na yenye tija katika mchakato wa kidemokrasia. Kupitia maonesho, nyimbo, na michezo ya maonesho, wasanii wanaweza kutoa ujumbe unaochochea mazungumzo ya kujenga, kuelimisha kuhusu haki za kiraia na kuhamasisha uwajibikaji wa viongozi kwa wananchi. Hii inasaidia kukuza mshikamano wa kitaifa na kuhakikisha sauti ya wananchi inasikika kwa uwazi na heshima.

Mwaka huu Tanzania itafanya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika Oktoba 2025. Hitaji la kuwa na mawasiliano ya kisasa, jumuishi, yanayoeleweka kwa urahisi na yenye athari chanya kwa jamii linazidi kuimarika. Katika kipindi hiki cha kisiasa ambacho huhusisha mijadala mikubwa kuhusu uongozi, uwajibikaji na mwelekeo wa taifa, Sanaa inajitokeza kama nyenzo yenye nguvu ya mawasiliano ambayo haiwezi kupuuzwa.

Kwa kutumia mbinu bunifu, lugha ya kipekee, hisia, burudani na ubunifu wa hali ya juu, Sanaa huwasilisha ujumbe kwa namna inayogusa fikra, mioyo na maisha ya watu wa makundi mbalimbali. Hii huifanya Sanaa kuwa jukwaa la kipekee la kuelimisha wananchi kuhusu haki zao za msingi, kuhamasisha ushiriki mpana wa makundi yote katika uchaguzi.  Wakati huohuo, Sanaa huwa ni chombo cha kuimarisha mshikamano wa kitaifa na kudhibiti misuguano ya kisiasa inayoweza kujitokeza.

Katika muktadha huu, makala hii inachunguza nafasi ya Sanaa na wasanii katika mchakato wa uchaguzi kwa mwaka 2025. Inaangazia namna ambavyo fani mbalimbali za Sanaa zinavyoweza kuchangia katika kujenga amani, kukuza ushiriki wa wananchi Katika mchakato mzima wa uchaguzi na kudumisha misingi ya demokrasia nchini Tanzania. .



**1. Sanaa Kama Chombo Madhubuti cha Elimu ya Uraia**

Wasanii wa fani mbalimbali wameendelea kutumia vipaji vyao kuelimisha umma juu ya haki na wajibu wa wananchi wakati wa uchaguzi. Huku Tume ya Taifa ya Uchaguzi ikiendeleza kampeni za elimu ya mpiga kura, Sanaa inaweza kuleta mageuzi ya kweli kwa njia zifuatazo.

- Kuibua mijadala kupitia maigizo ya kuigiza maisha halisi ya wapiga kura na wagombea.
- Kutumia muziki unaohamasisha ushiriki wa watu wote kwa amani na busara;
- Kuchapisha vibonzo, michoro na kazi za Sanaa za kuona zinazoeleza hatua za kupiga kura na kuepuka udanganyifu.

Katika kuelekea Oktoba 2025, Sanaa inaweza kufanikisha elimu ya uraia hasa kwa vijana na makundi yasiyofikiwa na njia rasmi.

**2. Sanaa Katika Kuimarisha Amani, Umoja na Mshikamano wa Kitaifa**

Historia ya chaguzi katika mataifa mengi ya Afrika imejaa mifano ya machafuko, ghasia za kisiasa, migawanyiko ya kijamii na hata kuvunjika kwa amani baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa. Migogoro hii mara nyingi hutokana na lugha za chuki, ushabiki uliopitiliza na ukosefu wa majukwaa ya kueleza tofauti kwa njia ya amani. Tanzania kwa zaidi ya miongo sita ya uhuru wake, imeendelea kujitambulisha kama kisiwa cha amani barani Afrika. Sifa hii inahitaji kulindwa, kudumishwa na kuendelezwa kwa nguvu zote, hasa katika vipindi vya uchaguzi ambavyo huambatana na hisia kali za kisiasa. Katika mazingira haya ya kihistoria na kisiasa, Sanaa inajitokeza kama daraja muhimu la kuunganisha jamii, kupoza jazba na kuhimiza maelewano. Wasanii wa muziki, maigizo, Sanaa za mikono, vibonzo na hata wachoraji, wana nafasi ya kipekee katika kueneza jumbe za utulivu, mshikamano na mapenzi ya nchi kupitia kazi zao za ubunifu. Mchango wa wasanii unaweza kuonekana katika maeneo yafuatayo:

Nyimbo zenye kauli mbiu zenye kuhimiza umoja zinazoelimisha juu ya madhara ya chuki, ukabila, udini au itikadi kali za kisiasa. Muziki unaotungwa na kutolewa wakati wa uchaguzi unaweza kuwa silaha ya amani inayopenya katika mioyo ya watu kwa haraka zaidi kuliko hotuba rasmi au mikutano ya kisiasa.

Ushairi na maigizo ya kisiasa yenye maadili, ambayo huonesha hadithi za maisha ya kawaida, changamoto zinazowakumba wananchi bila kujali chama chao na umuhimu wa kuheshimu tofauti za maoni kama sehemu ya ustaarabu wa kisiasa. Hii husaidia kuondoa hofu na kutoaminiana miongoni mwa wapiga kura na wafuasi wa vyama tofauti.

Kazi za Sanaa za mikono na maonesho ya wazi, kama vile maonesho ya picha au vibonzo vya kisiasa vinavyobeba ujumbe wa kitaifa, vinaweza kutumika kama jukwaa la mijadala ya kijamii kuhusu umuhimu wa kudumisha Tanzania moja, licha ya tofauti zetu za kisiasa, kikabila au kijamii.

Katika kipindi hiki nyeti kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025, ambapo teknolojia na mitandao ya kijamii vina nafasi kubwa katika kusambaza taarifa, mchango wa Sanaa katika kudhibiti lugha chafu, uvumi na uchochezi mtandaoni ni wa msingi kabisa. Wasanii wenye ushawishi mitandaoni wanaweza kutumia majukwaa yao kuhimiza mazungumzo yenye staha, kuhimiza heshima ya mchakato wa uchaguzi na kuwahimiza vijana ambao ni kundi lenye nguvu zaidi kisiasa kuwa mabalozi wa amani na mshikamano.

Kwa hivyo, Sanaa inapaswa kutazamwa si kama burudani tu, pia kama nguzo muhimu ya kuimarisha utulivu wa taifa katika nyakati za kisiasa, kwa sababu amani ndiyo msingi wa maendeleo endelevu na demokrasia ya kweli.



**3. Sanaa Kama Jukwaa la Kijumuishi kwa Makundi Maalum**

Wasanii wanaweza kusaidia kuhakikisha kuwa makundi maalum kama vile wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na jamii za pembezoni wanashiriki kikamilifu katika uchaguzi. Kwa mfano:

(i) Maudhui ya Sanaa yanayochochea wanawake kugombea na kushiriki katika maamuzi ya kisiasa.


(ii) Kampeni za wasanii maarufu mitandaoni zinazo hamasisha vijana waliojiandikisha kujitokeza kupiga kura.

(iii)Ubunifu wa kazi za Sanaa zenye lugha rahisi, alama au sauti kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa kusikia au kuona.

Hii inaendana na malengo ya kidemokrasia ya kuwa na ushiriki jumuishi, bila kubagua kundi lolote.

**4. Wasanii kama Mabalozi wa Demokrasia na Uwajibikaji**

Wasanii, hususan wale wenye ushawishi mkubwa katika jamii, wana nafasi ya kipekee katika kujenga jamii inayotambua thamani ya demokrasia na uwajibikaji wa viongozi. Katika jamii ya kisasa iliyojaa taarifa nyingi, sauti ya msanii maarufu ina uwezo wa kuvuta hisia za mamilioni ya watu kwa haraka, kwa kina na kwa njia ya kipekee kuliko njia nyingi rasmi za mawasiliano. Wasanii wanapozungumza, jamii husikiliza, si tu kwa sababu ya umaarufu wao, bali kwa sababu wana uwezo wa kuwasilisha ujumbe kwa lugha rahisi, ya kugusa na ya kuwavutia watu wa makundi mbalimbali.



Kuelekea Uchaguzi Mkuu wa 2025, wasanii wanaweza kuwa nguzo kuu ya kusukuma mbele ajenda ya uchaguzi huru, wa haki na wenye tija kwa taifa kwa njia mbalimbali zifuatazo:

Kuwa mabalozi wa kampeni za kupiga kura kwa amani, wakihamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kidemokrasia huku wakikemea vitendo vya vurugu, rushwa, uchochezi na ushawishi usio halali wa wapiga kura. Kupitia muziki, video fupi, tamthilia, mashairi na Sanaa ya mitandaoni, wasanii wanaweza kuendesha kampeni za amani zenye nguvu na ushawishi mkubwa, hasa kwa vijana ambao ni kundi lenye idadi kubwa ya wapiga kura.



Kushirikiana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), asasi za kiraia, vyombo vya habari na vyama vya siasa, ili kufikisha ujumbe mmoja wa kitaifa kuhusu uchaguzi wa haki, huru na wa amani. Ushirikiano huu unaweza kuchukua sura ya kampeni maalum za kitaifa, warsha za mafunzo kwa wasanii kuhusu elimu ya uraia, au kutunga kazi za pamoja zinazojenga uelewa na mshikamano miongoni mwa watanzania.

Katika zama hizi za kidijitali, ambapo mitandao ya kijamii imechukua nafasi kubwa ya mawasiliano, wasanii wamejipatia jukwaa lenye ushawishi mkubwa wa kijamii. Kupitia Instagram, TikTok, YouTube, Facebook na X (zamani Twitter), wanaweza kueneza ujumbe wa matumaini, mshikamano na mabadiliko chanya kwa mamilioni ya watanzania kwa haraka na kwa namna inayoeleweka kirahisi. Uwezo huu unapaswa kutumika ipasavyo kuhamasisha ushiriki wa kidemokrasia wenye misingi ya amani, heshima na maadili ya kitaifa.

Kwa msingi huo, ni muhimu sekta ya Sanaa ishirikishwe kikamilifu katika maandalizi na utekelezaji wa kampeni za uchaguzi. Wasanii si watazamaji wa mchakato wa kidemokrasia bali ni washiriki hai, wenye nafasi ya kipekee ya kugusa jamii kwa njia ya ubunifu. Kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025, Sanaa inapaswa kutambuliwa kama mshirika wa kweli katika kuimarisha demokrasia, mshikamano wa kitaifa na amani ya kudumu kwa maendeleo ya Taifa. Kwa uwezo wake wa kipekee wa kugusa mioyo, kuburudisha, kuelimisha na kuhamasisha kwa wakati mmoja, Sanaa inaweza kuwa sehemu muhimu ya mchakato wa uchaguzi, ikitoa dira kwa jamii kuelewa haki zao, kutambua wajibu wao, na kushiriki kikamilifu kwa njia ya amani na maadili. Wasanii, kupitia kazi zao, wanaweza kuwa mashujaa wa mabadiliko chanya, mabalozi wa amani, na walinzi wa maadili ya kisiasa.

Ni wajibu wa serikali, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, vyama vya siasa, mashirika ya kiraia, vyombo vya habari na jamii kwa ujumla kuwatambua na kuwashirikisha wasanii kwa dhati. Wasanii wasiwe tu watoa burudani pekee, bali kama wadau muhimu wa uchaguzi wa haki, huru na amani na wenye tija kwa maendeleo ya taifa letu. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumewekeza si tu katika uchaguzi bora, pia katika Tanzania yenye mshikamano, inayoheshimu sauti za wote na inayojenga msingi imara wa utawala bora kwa vizazi vijavyo.




## Rais Samia Aimarisha Ushirikiano Kupitia Urembo na Maendeleo




Mrembo wa Dunia 2025, Opal Suchata Chuangsri kutoka Thailand, na Mrembo wa Afrika 2025, Hasset Dereje Admassu kutoka Ethiopia, walitua nchini Tanzania. Miongoni mwa ziara walizozifanya nchini ni pamoja na kutembelea visiwa vya Zanzibar ambako walikutana na viongozi wakuu wa nchi kwa mazungumzo muhimu. Vikao hivyo, pamoja na mambo mengine vililenga kukuza ushirikiano wa kimataifa kupitia jukwaa la urembo na maendeleo endelevu.

Wakiwa visiwani Zanzibar, walimbwende hao walikutana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika Kijiji cha Kizimkazi, tarehe 20 Julai 2025. Katika mazungumzo na Mheshimiwa Rais, waliwasilisha miradi ya kijamii kupitia mpango wa "Beauty with a Purpose". Opal alielezea juhudi zake za kuelimisha jamii kuhusu saratani ya matiti nchini Thailand. Aidha, Hasset alieleza namna anavyowawezesha vijana wa kike kwa mafunzo ya ujuzi nchini Ethiopia.




Wakiwa visiwani Zanzibar, walimbwende hao walikutana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika Kijiji cha Kizimkazi, tarehe 20 Julai 2025. Katika mazungumzo na Mheshimiwa Rais, waliwasilisha miradi ya kijamii kupitia mpango wa "Beauty with a Purpose". Opal alielezea juhudi zake za kuelimisha jamii kuhusu saratani ya matiti nchini Thailand. Aidha, Hasset alieleza namna anavyowawezesha vijana wa kike kwa mafunzo ya ujuzi nchini Ethiopia.



Rais Samia aliwapongeza kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwa sauti ya mabadiliko chanya duniani, hususan kwa vijana wa kike. Alisisitiza umuhimu wa majukwaa ya kimataifa kama Miss World katika kuendeleza diplomasia ya utamaduni na kuhamasisha maendeleo endelevu. Aliwazawadia warembo hao zawadi za asili zenye utambulisho wa utamaduni wa Zanzibar zikiwemo viungo vya asili na kutoa mwaliko wa wazi wa kurejea tena nchini Tanzania.






Miongoni mwa waliohudhuria kikao hicho ni Opal na Hasset, ambapo Rais Mwinyi alisifu mchango wao katika kutangaza masuala ya kijamii na kutumia umaarufu wao kuhamasisha maendeleo. Alisisitiza umuhimu wa kuitangaza Zanzibar kupitia jukwaa la Miss World na kuahidi ushirikiano wa karibu. Bi. Morley alipokea zawadi maalum kutoka kwa Rais Mwinyi kama ishara ya heshima na mashirikiano.

Mrembo wa Dunia 2025, Bi Suchata “Opal” Chuangsri kutoka Thailand, pamoja na Miss World Africa 2025, Bi Hasset Dereje kutoka Ethiopia, waliwasili nchini Tanzania kwa ziara maalum iliyolenga kutembelea vivutio vya utalii. Vilevile, walipanga kutembelea taasisi muhimu za sanaa na utamaduni zinazochangia kukuza urithi wa utamaduni na vipaji vya vijana nchini. Ziara hiyo imekuwa fursa muhimu ya kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika sekta za utalii, sanaa na utamaduni, sambamba na kuendeleza mahusiano ya utamaduni kati ya Tanzania na mataifa mengine

Miss World 2025, Bi Suchata “Opal” Chuangsri, aliwasili nchini Tanzania tarehe 15 Julai 2025 kupitia Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam, ambako alipokelewa na Mkurugenzi wa Sanaa kutoka Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo Dkt. Emmanuel Ishengoma, Katibu Mtendaji wa BASATA, Dkt. Kedmon Mapana pamoja na viongozi wengine wa serikali na taasisi za utalii, wakiwemo maafisa wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB).

Akizungumza baada ya mapokezi hayo, Dkt. Ishengoma, alisema kuwa ujio wa Miss World ni fursa adhimu kwa Tanzania kujitangaza kimataifa kupitia taswira ya mrembo huyo ambaye ni mfano wa uzuri, uelewa na ushawishi wa kimataifa. Aliongeza kuwa ziara hiyo ni sehemu ya juhudi za serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya utalii na sanaa katika kuitangaza Tanzania kama kivutio bora cha utalii barani Afrika na duniani kwa ujumla.




Siku moja baada ya kuwasili, mnamo Julai 16, 2025, Miss World Opal aliambatana na mshindi wa pili wa taji hilo duniani na pia Miss World Africa 2025, Bi Hasset Dereje kutoka Ethiopia, kutembelea makao makuu ya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). Ziara hiyo ilikuwa sehemu ya mpango maalum wa kuwafahamisha wageni hao umuhimu wa sanaa na utamaduni wa Kitanzania katika maendeleo ya jamii na uchumi.




Warembo hao walipata fursa ya kukutana na viongozi mbalimbali wa sanaa, kutembelea ofisi na vitengo vya BASATA, pamoja na kushuhudia shughuli za ukuzaji wa vipaji vya vijana kupitia programu za mafunzo na matamasha. Viongozi wa BASATA waliwapatia maelezo ya kina kuhusu jukumu la baraza hilo katika kusimamia, kukuza na kuendeleza sekta ya sanaa nchini Tanzania.




Akizungumza katika ziara hiyo, Bi Opal alisema amevutiwa sana na namna Tanzania inavyothamini na kuendeleza sanaa, utamaduni na vipaji vya vijana. Alisema kuwa aliguswa na ari, ubunifu na mchango wa wasanii wa Kitanzania katika kuibua matumaini mapya kwa vizazi vijavyo kupitia kazi zao za sanaa.

Bi Opal aliongeza kuwa uzoefu alioupata nchini Tanzania umemgusa kwa namna ya kipekee, na akaahidi kuwa balozi wa hiari wa kuitangaza Tanzania kimataifa. Alisisitiza kuwa utajiri wa kitamaduni, ukarimu wa watu na uzuri wa mazingira ya Tanzania ni hazina ambayo dunia inapaswa kuifahamu na kuithamini.

# MPANGO MKAKATI WA BASATA




## BASATA Yajipanga Kuibadili Tasnia ya Sanaa kwa Msingi wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050

Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) linatarajia kuzindua Mpango Mkakati Mpya wa Miaka Mitano (2025/26–2029/30) unaolenga kuleta mageuzi ya kweli katika sekta ya sanaa nchini Tanzania. Mpango huu umebuniwa kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa kama vilivyoainishwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, ambayo inalenga kuijenga Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu, inayotegemea ubunifu, viwanda na jamii yenye mshikamano.

Kupitia mpango huu mpya, BASATA inalenga kuimarisha miundombinu ya sanaa, kukuza ubunifu na matumizi ya teknolojia, pamoja na kutoa fursa za mafunzo na masoko kwa wasanii wa ndani na wale wa nje ya miji mikuu. Mfumo wa kisasa wa kidijitali wa usimamizi wa wasanii (AMIS) utarahisisha huduma za usajili, leseni na taarifa muhimu kwa wasanii, ikiwa ni hatua ya kuendana na dira ya kujenga jamii yenye umahiri wa kidijitali ifikapo mwaka 2050.Dira ya 2050 inaelekeza Taifa kuwa jumuishi, lenye ustawi na linalojitegemea. Katika hilo, BASATA kupitia mpango wake mpya, inaweka msisitizo kwenye usawa wa kijinsia, uboreshaji wa maadili ya sanaa, uwezeshaji wa vijana na watu wenye ulemavu, pamoja na kuhamasisha uwekezaji kupitia ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP).

Mpango huu mpya wa BASATA umeandaliwa kwa ushirikishwaji mkubwa wa wadau wa sanaa, mashirika ya serikali, taasisi binafsi, wanataaluma, na wasanii wenyewe. Ukijengwa juu ya tathmini ya mpango uliopita na viashiria vya maendeleo ya sekta ya ubunifu, mpango huu unaweka vipaumbele vitano vya kimkakati, ambavyo ni:

1.Kuboresha huduma za afya na kupunguza maambukizi ya UKIMWI na magonjwa yasi yoambukiza kwa wasanii.

2.Kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Rushwa na kukuza utawala bora.

3.Kuendeleza ubunifu wa kisanaa, ujuzi wa kitaaluma na maendeleo ya kitaaluma kwa wasanii.

4.Kuimarisha ushirikiano na ushiriki wa wadau wa sanaa ndani na nje ya nchi.

5.Kujenga uwezo wa taasisi, miundom binu, na mifumo ya usimamizi wa sanaa..



Kwa mujibu wa Katibu Mtendaji wa BASATA, Dkt. Kedmon Mapana, mpango huu umejengwa katika msingi wa Ushirikiano, Uwazi, Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali. Lengo ni kuhakikisha kuwa sanaa inachangia kikamilifu katika ajenda ya maendeleo ya kitaifa. “Tunalenga kuiweka Tanzania katika ramani ya dunia kama kitovu cha ubunifu, sanaa bora na utambulisho wa kiutamaduni,” alisema Dkt. Mapana. Kwa wadau wa sanaa,

Aidha,Mpango Mkakati huu unatarajiwa kuleta manufaa makubwa kwa kuwa unalenga kuimarisha mazingira wezeshi kwa wasanii kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi. Kupitia utekelezaji wa mifumo ya kisasa ya kidijitali kama vile mfumo wa usimamizi wa wasanii (AMIS), wasanii watapata huduma za usajili, leseni na taarifa muhimu kwa urahisi zaidi. Aidha, mpango huu unatoa kipaumbele kwa uboreshaji wa miundombinu ya sanaa katika ngazi ya mikoa.



Mpango Mkakati huo unalenga kuwepo kwa vituo vya sanaa vya kikanda ambavyo vitasogeza huduma karibu na wadau walioko nje ya miji mikuu. Kwa kushirikiana na taasisi za elimu na wahisani wa kimataifa, mpango huu pia utasaidia kutoa mafunzo na ujenzi wa uwezo kwa wasanii, huku ukilenga kuongeza uelewa juu ya masuala ya mikataba, hakimiliki na usimamizi wa kazi za sanaa. Vilevile, BASATA imejipanga kukuza masoko ya kazi za sanaa ndani na nje ya nchi kwa kutumia diplomasia ya kiutamaduni na kushiriki katika maonyesho na matamasha ya kimataifa. Kwa njia hii, wasanii wa Tanzania watapata fursa zaidi za kiuchumi, kushiriki katika majukwaa ya kimataifa, na kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya taifa kupitia sanaa na ubunifu.

Mpango Mkakati huu pia unalenga kuongeza mapato ya ndani ya Baraza, kupanua huduma hadi ngazi za kanda kwa kupitia ofisi mpya za kanda. Pia, kuanzisha mfumo wa usajili na leseni wa kidijitali (AMIS), pamoja na kushirikiana na taasisi za elimu na wafadhili wa kimataifa kwa ajili ya mafunzo na fursa za kimataifa kwa wasanii.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza, Prof. Saudin Mwakaje, alisisitiza kuwa mpango huu unaakisi dhamira ya dhati ya BASATA katika kujenga mifumo endelevu ya sanaa nchini. “Sanaa ni nguzo muhimu ya utambulisho wa taifa, mshikamano wa kijamii na maendeleo ya kiuchumi,” alibainisha Prof. Mwakaje.

Kwa mara ya kwanza, mpango huu unaweka msisitizo mkubwa Katika; **- Ujumuishi wa Kijinsia, Maadili ya Sanaa, Uwezeshaji wa Vijana na Usimamizi wa Kazi za Sanaa za Kidijitali.** Pia, unalenga kuhamasisha uwekezaji kutoka sekta binafsi kupitia mikakati ya PPP (Public-Private Partnerships).

Kupitia Mpango Mkakati huu mpya, BASATA inalenga kuandika ukurasa mpya wa mafanikio ya sekta ya sanaa Tanzania, ikitoa jukwaa la kitaifa na kimataifa kwa wasanii kujieleza, kushiriki, na kunufaika kiuchumi na kijamii kupitia kazi zao za ubunifu.

# DKT. MAPANA ASHINDA KWA KISHINDO

## Dkt. Mapana, Kiongozi wa Sanaa Anayetambulika Kimataifa



Katika hatua ya kihistoria inayodhihirisha ushawishi na mchango mkubwa wa Tanzania katika masuala ya utamaduni duniani, Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Dkt. Kedmon Mapana, amechaguliwa rasmi kuiwakilisha Tanzania katika Kamati Jumuishi ya Kiserikali ya UNESCO inayosimamia utekelezaji wa Mkataba wa 2005 wa Kulinda na Kuendeleza Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni.

Uchaguzi huo ulifanyika tarehe 20 Juni 2025 makao makuu ya United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO) yaliyopo Paris nchini Ufaransa. Ushindi wa Dkt. Mapana unatazamwa kama ushindi mkubwa kwa taifa la Tanzania. Hii siyo tu kwa kutambua juhudi za serikali katika kukuza na kulinda utamaduni wa nchi, pia kwa kuthibitisha uwezo wa wataalamu wake kushiriki kikamilifu katika majukwaa ya kimataifa ya maamuzi. Nafasi hii kwa Dkt. Mapana inatarajiwa kuimarisha nafasi ya Tanzania katika masuala ya utungaji sera za kimataifa kuhusu utamaduni, kubadilishana uzoefu na nchi nyingine na kufungua fursa zaidi za ushirikiano wa kimataifa kwa wasanii na wadau wa sanaa na utamaduni.

Kupitia nafasi hii, Tanzania imeingia kwenye meza ya majadiliano ya kimataifa kuhusu masuala nyeti ya utamaduni, ubunifu na haki ya jamii mbalimbali kujieleza kwa uhuru wa kiutamaduni. Nchi sasa inajumuika na mataifa yenye nguvu ya kimkakati kwenye sekta ya utamaduni kama vile Belgium, Sweden, Armenia, Azerbaijan, Brazil, Colombia, Philippines, Viet Nam, Mauritania, Djibouti na Tunisia. Ushindi huu ni heshima kubwa kwa taifa, wasanii na wadau wa utamaduni nchini.

UNESCO ni shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na masuala ya elimu, sayansi na utamaduni, likiwa na jukumu muhimu la kulinda na kuendeleza urithi wa tamaduni duniani. Kupitia mikutano ya wanachama wa mkataba wa 2005, UNESCO huleta pamoja nchi mbalimbali ili kujadili na kutathmini mafanikio na changamoto za kulinda utamaduni wa aina zote ikiwemo “tangible” (mali zinazoonekana kama majengo na kazi za sanaa) na “intangible” (urithi usioonekana kama mila, desturi na lugha). Tanzania, kwa kushiriki katika Kamati ya Kiserikali (Intergovernmental Committee) inayoundwa na wajumbe 24, ina nafasi ya kipekee kuonekana kimataifa, kuvutia wadau wa maendeleo na kushirikiana na nchi nyingine kulinda na kukuza tamaduni zake.

Katika ziara hiyo muhimu, Dkt. Mapana aliambatana na Dkt. Emmanuel Ishengoma, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Sanaa, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ambapo wote kwa pamoja walishiriki majadiliano ya kitaifa na kimataifa kuhusu mustakabali wa sekta ya sanaa na utamaduni duniani.



Dkt. Kedmon Mapana ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), taasisi ya serikali inayosimamia, kuendeleza na kulinda sekta ya sanaa nchini Tanzania. Katika nafasi hii, Dkt. Mapana anaongoza juhudi za kuimarisha mazingira ya wasanii, kukuza ubunifu na kuhakikisha sanaa inachangia kikamilifu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya taifa.

Kabla ya kuteuliwa BASATA, Dkt. Mapana alikuwa Mhadhiri Mwandamizi wa Muziki katika Idara ya Sanaa za Ubunifu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambako alihusika katika kufundisha, kufanya tafiti na kuratibu shughuli za kukuza sanaa za utamaduni. Ana shahada ya kwanza ya Muziki kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Shahada ya Uzamivu (PhD) katika Elimu kutoka Chuo Kikuu cha Seattle Pacific, Marekani, ambako alitunukiwa Tuzo ya Rais (President's Citation) kwa mchango wake wa kipekee katika jamii na taaluma.

Mbali na taaluma ya ufundishaji, Dkt. Mapana ni mwanzilishi wa Tamasha la Muziki wa Cigogo, ambalo linaadhimisha zaidi ya muongo mmoja wa kuenzi utamaduni wa Wagogo. Pia ni mmoja wa wakurugenzi wa Chamwino Arts Centre (CAC), shirika lisilo la kiserikali linalojihusisha na kuhifadhi na kukuza utamaduni kupitia sanaa ya ngoma. CAC ni zao la maono ya Dkt. Mapana, ambaye alikulia Chamwino, miongoni mwa jamii ya Wagogo waliotumia ngoma kama njia ya mawasiliano, elimu, urithi na utambulisho wa kijamii.

Kwa ujumla, Dkt. Mapana ni mtafiti, msanii na kiongozi wa kijamii ambaye kazi zake zimejikita katika kuinua jamii kupitia sanaa, kuenzi utamaduni wa Kitanzania, na kuwawezesha vijana kutumia sanaa kama nyenzo ya maendeleo.

Tangu kuteuliwa kwake BASATA, Dkt. Mapana ameanzisha mageuzi makubwa ya kimuundo na kimkakati ndani ya Baraza akilenga kuimarisha mazingira ya ubunifu, hakimiliki, ushirikiano wa kimataifa na utafiti wa kisanaa. Kupitia ushiriki wake katika kamati ya UNESCO, Tanzania itakuwa na nafasi ya kushiriki katika kutunga miongozo, sera na miradi ya kimataifa ya utamaduni, na hivyo kuwezesha wasanii wa kitanzania kushiriki kikamilifu kwenye majukwaa ya dunia.

Kupitia nafasi hii mpya, Dkt. Mapana anakuwa kiungo muhimu kati ya Tanzania na jukwaa la utamaduni wa dunia. Ushiriki wake unatarajiwa kuimarisha sauti ya Tanzania katika ajenda za kimataifa kuhusu sanaa na utamaduni, na kuongeza ushawishi wa nchi katika mipango ya maendeleo ya sekta hii muhimu. BASATA inampongeza Dkt. Mapana kwa ushindi huu mkubwa unaodhihirisha ubora wa wataalamu wa sanaa nchini Tanzania na kutufungua kwenye fursa zaidi za kimataifa.




## Nguvu ya Ubunifu wa Sanaa Katika Kuleta Mabadiliko Chanya

Mbele ya jukwaa dogo la kijiji cha Nyamongo wilayani Tarime, kijana aitwaye Juma, akiwa na kikundi chake cha maigizo, alisimama akiwa amevaa mavazi ya kuigiza ya mtu aliyenyanyaswa. Aliigiza hadithi ya msichana mdogo aliyepitia ukatili wa kijinsia lakini akapata msaada kupitia kampeni ya sanaa iliyofika kijijini mwao. Tamthilia hiyo, iliyoandaliwa chini ya mwamvuli wa mpango wa "Sanaa kwa Maendeleo ya Jamii", iliwagusa wengi kwa kiasi kikubwa ambapo watu walilia, walitafakari na hata baadhi ya viongozi wa jamii walichukua hatua. Hii ndiyo nguvu halisi ya sanaa katika kuhamasisha mabadiliko kupitia simulizi zenye uhai na mguso wa moja kwa moja kwa jamii.

Kupitia kazi za uchoraji, muziki, filamu, ngoma na mashairi, wasanii wengi kama Juma wamekuwa mabalozi wa ujumbe muhimu wa kijamii, wakitoa elimu bila kutumia maneno mengi au lugha rasmi. Huko Mwanza, msichana aitwaye Rehema alitumia uchoraji wake kuonyesha hadithi ya vijana waliotelekezwa na jamii lakini wakapata matumaini kupitia vikundi vya sanaa. Mchoro wake uliwekwa kwenye maonesho ya vijana yaliyoandaliwa na wadau wa sanaa. Baadaye, alialikwa kuzungumza mbele ya viongozi wa serikali kuhusu changamoto zinazowakumba vijana mitaani. Hii ni mifano ya wazi ya namna sanaa inavyobeba sauti ya wanyonge na kuibua mijadala yenye tija.

Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), kwa kutambua uwezo huu mkubwa wa sanaa katika kusimulia na kuibua hisia halisi, linaendelea kuwahamasisha wasanii kutumia vipaji vyao kama chombo cha mabadiliko chanya. Katika warsha na makongamano mbalimbali, BASATA huwapatia wasanii zana, mbinu na miongozo ya namna ya kutumia sanaa kuhamasisha mijadala kuhusu haki za binadamu, afya ya akili, mazingira, maadili na maendeleo ya jamii kwa ujumla. Tofauti na maelezo ya moja kwa moja, sanaa huingia moja kwa moja moyoni, huibua tafakari ya kina na mara nyingi husababisha hatua ya kweli kuchukuliwa.

Katika ulimwengu wa sasa unaokabiliwa na changamoto nyingi, simulizi zinazowasilishwa kupitia sanaa haziwezi kupuuzwa. Ni kupitia hadithi za Juma na Rehema pamoja na maelfu ya wasanii wengine nchini, ambapo jamii hupata nafasi ya kutafakari upya maisha yao, kuhoji hali halisi na kuchukua hatua. Hadithi hizi za kisanaa hubeba maana pana zinagusa maisha, zinapaza sauti zisizo na jukwaa, na huchochea mabadiliko hata katika ngazi ya familia na jamii nzima

Kwa karne nyingi, jamii za kiafrika zimekuwa zikihifadhi historia, maarifa na maadili kupitia sanaa. Ngoma za asili, mavazi ya kitamaduni, mapambo ya mwili, mashairi na methali vimekuwa sehemu ya simulizi zinazohifadhi na kuendeleza utambulisho wa kijamii. BASATA, kama chombo cha serikali kinachosimamia sekta ya sanaa nchini Tanzania, kina jukumu la kuhakikisha kuwa urithi huu wa kisanaa unalindwa, unathaminiwa na kuendelezwa. Hii ni pamoja na kuratibu matamasha ya sanaa na utamaduni ambayo huwakutanisha wasanii kutoka mikoa mbalimbali kuwasilisha hadithi za jamii zao kupitia ngoma, muziki wa asili na maigizo.



Katika enzi hii ya kidijitali, wasanii wana nafasi kubwa zaidi ya kusambaza hadithi zao kwa haraka na kwa hadhira pana kupitia majukwaa kama YouTube, Instagram, TikTok na Spotify. Hali hii imepanua wigo wa uhadithi wa kisanaa, hasa kwa vijana wanaotumia mbinu bunifu kushiriki simulizi zao. Mfano wa msanii Zuhura Othman Soud, maarufu kama Zuchu, ambaye anatumia muziki wake kuwasilisha hadithi za mapenzi, ujasiri na utambulisho wa mwanamke wa Kiswahili, unaonesha namna sanaa inavyoweza kuwa daraja la mawasiliano ya kina hata katika karne ya 21. Mafanikio haya yanadhihirisha kuwa sanaa ni njia madhubuti ya kuwasilisha simulizi zenye mguso na athari katika jamii ya sasa.

Hadithi zinazowasilishwa kupitia sanaa zina uwezo mkubwa wa kugusa nafsi, kuibua fikra na kuchochea mabadiliko ya kijamii. Kila igizo, mchoro au wimbo hubeba simulizi linaloangazia hali halisi ya maisha ya watu na changamoto zao. Mfano wa Juma na Rehema ni ushahidi tosha kuwa sanaa si burudani tu, pia ni chombo cha elimu, uhamasishaji na mabadiliko. Wasanii hawa, na maelfu ya wengine nchini, wamekuwa mabalozi wa sauti zisizosikika, wakisimulia simulizi za matumaini, ujasiri na mabadiliko kupitia vipaji vyao vya kipekee.

BASATA inaendelea kuwa kinara katika kuhakikisha kuwa sanaa inatumika kama nguvu ya maendeleo. Kwa kuandaa warsha, makongamano na kutoa miongozo ya maadili, Baraza huwajengea wasanii uwezo wa kutumia sanaa kwa njia zenye tija kijamii. Kupitia usimamizi na uhamasishaji wake, BASATA linawahimiza wasanii kuwa sauti ya jamii kuhusu masuala nyeti kama haki za binadamu, afya ya akili, mazingira na maadili. Katika muktadha huu, sanaa inageuka kuwa daraja la mawasiliano kati ya wananchi na maendeleo na BASATA linahakikisha daraja hilo linakuwa imara, lenye uadilifu, na linaloleta matumaini kwa taifa zima



# SANAA NA ONGEZEKO LA PATO LA TAIFA

## Mchango wa Sekta ya Sanaa Katika Pato la Taifa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameeleza kwa fahari mafanikio makubwa yanayoshuhudiwa katika sekta ya sanaa nchini. Akiwasilisha takwimu zenye kutia matumaini, Mheshimiwa Rais alisema kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la wasanii wa ndani wanaopata vibali vya kwenda nje ya nchi kwa ajili ya shughuli za kisanaa. Idadi ya vibali hivyo imeongezeka kutoka 122 mwaka 2020 hadi kufikia 1,492 mwaka 2024, hatua inayodhihirisha jinsi sanaa ya Tanzania inavyoendelea kuvuka mipaka na kupata kutambulika kimataifa.

Alisema hayo tarehe 12 Juni 2025, wakati wa kuvunja Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bungeni jijini Dodoma. Katika hotuba hiyo, Mheshimiwa Rais alibainisha pia kuwa vibali vya wadau wa sanaa kuingiza wasanii kutoka nje ya nchi vimeongezeka kutoka 75 hadi 625 katika kipindi hicho hicho. Ongezeko hilo linaonesha kuimarika kwa mazingira ya kisanaa nchini na kuongezeka kwa fursa za ushirikiano wa kimataifa katika tasnia ya sanaa na burudani.Akihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Dodoma, tarehe 28 Juni 2025, wakati wa kuhitimisha Bunge hilo kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Madiwani, Wabunge na Rais, Mhe. Samia alisisitiza kuwa sekta ya sanaa ni mhimili unaochochea maendeleo ya watu, utamaduni, teknolojia, na uchumi wa Taifa.



Vilevile, takwimu nyingine muhimu kuhusu mchango wa sekta ya sanaa katika pato la taifa, zilizowasilishwa bungeni jijini Dodoma tarehe 22 Juni 2025, na Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo (Mb.), Waziri wa Mipango na Uwekezaji. Tawimu hizi zimedhihirisha kwa mara ya kwanza kuwa sekta ya sanaa na burudani ndiyo iliyokuwa na kasi ya juu zaidi ya ukuaji nchini Tanzania. Kwa mujibu wa takwimu hizo, sekta hiyo ilichangia ukuaji wa uchumi kwa asilimia 17.1 mwaka 2024, ikiwa ndiyo kiwango cha juu zaidi kuliko sekta nyingine zote. Hii ni ishara ya wazi kuwa sanaa na burudani si tu chanzo cha ajira na vipato, pia ni

Kwa muktadha huu, sekta ya sanaa imeendelea kujidhihirisha kama kitovu cha maendeleo ya watu, ubunifu, uwekezaji na utambulisho wa kitaifa. Hali hii inaakisi kwa vitendo maono ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 pamoja na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), ambayo yote inatambua mchango wa sanaa kama nguvu ya uchumi na utamaduni wa Taifa.





Kwa muda mrefu, sekta ya sanaa ilikuwa haionekani kwa uwazi katika takwimu za kitaifa, huku mchango wake ukiwa umefungwa kwenye takwimu za sekta nyingine kama burudani, utalii au biashara ndogo ndogo. Hata hivyo, mwaka 2024 umeibua ukweli mpya kuwa sanaa siyo tena sekta ya pembeni bali ni kiongozi wa ukuaji wa uchumi. Kwa mujibu wa hotuba ya Waziri wa Mipango na Uwekezaji, sekta tano zilizokua kwa kasi ni kama zifuatavyo;-

1. Sanaa na Burudani – 17.1%
2. Uzalishaji na Usambazaji wa Umeme – 14.4%
3. Habari na Mawasiliano – 14.3%
4. Afya – 10.1%
5. Fedha na Bima – 9% hadi 13.8%

Uchumi kwa ujumla ulikua kwa asilimia 5.5%, ukichochewa na miradi mikubwa ya kimkakati, hasa miundombinu ya nishati, lakini sanaa imesimama juu kwa ubunifu, kipato na ajira.

Katika mafanikio haya, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) limeendelea kutoa msukumo muhimu katika kukuza mazingira rafiki kwa wasanii na wabunifu. Kupitia sera za kisasa, mifumo ya kidijitali na usimamizi wa kitaalamu, BASATA limewezesha kufanya usajili wa wasanii na kazi zao kwa njia ya mtandao; utoaji wa vibali vya kazi za sanaa kwa haraka na kwa uwazi; kushirikiana na taasisi kama COSOTA, Bodi ya Filamu, na Ofisi ya Taifa ya Takwimu National Bureau of Statistics). Pia, uboreshaji wa mazingira ya usimamizi juu ya uzingatiaji wa maadili katika kazi za Sanaa.

Kauli mbiu ya BASATA ya "Sanaa ni Ajira, Uchumi na Biashara" imeanza kutafsiriwa kwa vitendo kupitia mamilioni ya ajira zisizo za moja kwa moja na mitandao ya biashara ya sanaa inayovuka mipaka ya kitaifa. Sekta ya sanaa si ajira pekee kwa waigizaji, waimbaji, wachoraji, wabunifu wa mavazi, au watayarishaji wa filamu. Huu ni mfumo mpana unaogusa uzalishaji wa maudhui, utalii wa kitamaduni, tamasha za kimataifa, bidhaa za ubunifu na hata teknolojia.

Utafiti unaonesha kuwa sekta ya sanaa imekuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Sanaa imeweza kuzalisha maelfu ya ajira kupitia matamasha, maonesho ya sanaa na uzalishaji wa filamu. Kwasasa wabunifu wa mitindo ya mavazi wameanzisha kampuni zinazouza bidhaa zao hadi nje ya nchi, huku muziki wa kizazi kipya kama Bongo Fleva ukiendelea kuingiza mapato kupitia YouTube, majukwaa ya kidijitali na mifumo ya leseni. Wasanii hawa si waburudishaji tu, bali ni mawakala wa uchumi, walimu wa jamii na mabalozi wa taifa katika jukwaa la kimataifa. Pamoja na mafanikio haya, bado kuna changamoto ya msingi kama vile ukosefu wa takwimu mahsusi za kisekta.

Ili kutambua na kupima kwa kina mchango wa sanaa katika maendeleo ya taifa, kuna umuhimu wa kuanzisha tafiti maalum kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), ili kupata data sahihi na za kutegemewa. Sambamba na hilo, ni muhimu kujenga mifumo thabiti ya ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za kipato kinachotokana na shughuli za kisanaa. Serikali na wadau wanapaswa kuwezesha uanzishwaji wa kongani za viwanda vya ubunifu (creative hubs) zitakazochochea ajira na ubunifu, pamoja na kufungua masoko zaidi ya ndani na nje kwa kutumia diplomasia ya sanaa kama njia ya kukuza ushawishi wa kiutamaduni na kiuchumi duniani.

BASATA inapoendelea na mazungumzo na wadau mbalimbali wa sekta ya sanaa, serikali na mashirika ya kimataifa kuhusu uanzishwaji wa Kituo cha Taifa cha Takwimu za Sanaa. Katika kutekeleza mpango huu ni lazima kuhakikisha kunakuwepo na ushirikiano mpana na wa karibu kwa wahusika wote. Ushirikiano huu utahakikisha takwimu zinazokusanywa ni za kina, sahihi na zinakidhi mahitaji halisi ya sekta. Aidha, BASATA imeanza kuwekeza katika teknolojia za kisasa za ukusanyaji na uchambuzi wa data ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa wakati halisi na kwa ufanisi zaidi.

# UJENZI WA SANAA IMARA



## Safari ya Kujenga Taifa Lenye Utambulisho Madhubuti

Katika ulimwengu wa leo unaobadilika kwa kasi, sanaa sio tu burudani bali ni chombo kikuu cha maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Katika muktadha wa Tanzania, wasanii wameendelea kuwa nguzo ya kuendeleza sanaa imara inayowakilisha maadili, ndoto na historia ya taifa. Kupitia kazi zao wasanii wanashiriki moja kwa moja katika kujenga msingi wa taifa lenye utambulisho thabiti, mshikamano wa kijamii na fursa za kiuchumi.

Wasanii ni mabalozi wa tamaduni na sauti ya jamii kwa kutumia vipaji vyao kupitia filamu, muziki, sanaa za maonesho, fasihi andishi, mashairi, uchoraji na sanaa nyingine za ubunifu, wanaibua maudhui yenye jumbe nzito za kuelimisha, kuonya na kuburudisha jamii. Kazi zao huibua mijadala ya kijamii na kuhamasisha mabadiliko ya fikra na mitazamo miongoni mwa wananchi.

Kwa mfano, kupitia nyimbo zenye maudhui ya uzalendo, wasanii wamechangia kujenga hisia za utaifa, heshima kwa viongozi na kuthamini amani ya nchi. Maigizo na filamu zenye ujumbe kuhusu haki za binadamu, umuhimu wa elimu kwa watoto wa kike na wa kiume, vita dhidi ya rushwa na mapambano dhidi ya magonjwa kama UKIMWI, malaria na magonjwa ya akili, zimeleta uelewa mpana katika jamii na kuongeza uwajibikaji wa mtu binafsi.

Aidha, wasanii huchora taswira ya historia ya taifa, mashujaa wa zamani na simulizi za kizazi kwa kizazi, hivyo kuhifadhi utambulisho wa kitaifa na kurithisha mila kwa vizazi vijavyo. Hili husaidia taifa kuwa na dira na misingi imara ya kimaadili. Kwa ujumla, wasanii wanashikilia nafasi ya pekee kama walimu wa jamii kwa kutumia lugha rahisi na zenye mvuto.

Sekta ya sanaa imejidhihirisha kama mhimili muhimu wa uchumi unaokua, hususan katika kuzalisha ajira kwa vijana. Wasanii wanapojihusisha na kazi zao za ubunifu kama vile muziki, filamu, uchoraji, sanaa za maonesho na mitindo ya mavazi, hujenga minyororo ya thamani inayovuta wadau mbalimbali. Kupitia kazi moja ya sanaa, huibuka nafasi za ajira kwa watayarishaji wa muziki na filamu, wapiga picha, waongozaji wa matukio, wabunifu wa mavazi na jukwaa, mafundi mitambo, wahariri wa video, pamoja na wasambazaji wa kazi hizo sokoni. Ajira hizi huibuka si tu mijini bali pia vijijini ambako vipaji vingi huibuliwa na kukuzwa.

Kwa mujibu wa takwimu kutoka kwenye taarifa za uchumi wa taifa, sekta ya sanaa na ubunifu imekuwa miongoni mwa sekta zinazochangia kwa kasi katika pato la taifa, ikiwa ni kiashiria cha nafasi ya wasanii katika uchumi wa kisasa. Ongezeko la matamasha, maonesho ya kazi za sanaa, matumizi ya majukwaa ya kidijitali na uuzaji wa kazi za sanaa kimataifa vimeongeza mapato kwa wasanii na serikali kwa ujumla kupitia kodi na tozo mbalimbali. Hii inaonesha kuwa uwekezaji katika sekta ya sanaa si wa kijamii pekee, bali pia ni mkakati wa kiuchumi wenye tija katika kupambana na changamoto ya ajira na kuinua kipato cha wananchi.



## Kujenga Misingi ya Uongozi Bora wa Sekta

Katika muktadha wa mageuzi ya sekta ya sanaa, wasanii wameanza kujitokeza kama viongozi na waratibu wa shughuli mbalimbali za kisanaa. Hili limechochewa na uhitaji wa kuwa na usimamizi madhubuti wa kazi za sanaa pamoja na ulinzi wa haki za wasanii. Kupitia vyama, taasisi na mashirikisho ya kisanaa, wasanii wameweza kujipanga kwa pamoja ili kusimamia shughuli zao kwa weledi zaidi na kuhakikisha kuwa kazi zao zinalindwa kisheria dhidi ya wizi wa kazi za ubunifu.

Zaidi ya hilo, vyama hivi vimekuwa jukwaa muhimu la utetezi wa maslahi ya wasanii katika ngazi za kitaifa na kimataifa. Vimewezesha wasanii kushiriki katika mijadala ya sera, kushirikiana na taasisi za serikali na sekta binafsi, na kutoa maoni kuhusu sheria na miongozo inayoathiri tasnia yao. Hii ni hatua muhimu katika kujenga msingi imara wa uongozi bora ndani ya sekta ya sanaa, ambapo wasanii siyo tu watendaji pia watoa maamuzi kuhusu mustakabali wa kazi zao na maendeleo ya tasnia kwa ujumla.

## Sanaa Katika Kuchochea Mabadiliko ya Kijamii

Wasanii wameendelea kuwa sauti ya jamii kwa kutumia vipaji vyao kuibua hoja nyeti na kuchochea mabadiliko ya kijamii. Kupitia maigizo, muziki, mashairi, vichekesho na sanaa za picha wasanii huwasilisha jumbe zinazogusa maisha ya kila siku ya wananchi. yapo maudhui yanayotolewa kuhusu jamii kama vile unyanyasaji wa kijinsia, matumizi ya dawa za kulevya, ukatili wa majumbani na rushwa, hivyo yamekuwa yakitumika kuelimisha jamii na kuhamasisha maadili bora na uwajibikaji.

Mbali na kutoa burudani, sanaa imekuwa daraja la mawasiliano baina ya serikali, mashirika ya kiraia na wananchi. Wasanii hutumia sanaa kama njia ya kufikisha ujumbe wa kampeni za afya, elimu, mazingira na haki za binadamu. Kwa kufanya hivyo, wanachochea mijadala ya wazi miongoni mwa jamii, kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu masuala muhimu na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kuleta mabadiliko chanya ya kijamii

## Kufanikisha Mageuzi ya Kidijitali katika Sanaa



Katika enzi ya mapinduzi ya kidijitali, wasanii nchini Tanzania na duniani kwa ujumla wamepata fursa ya kipekee ya kujiendeleza kupitia matumizi ya majukwaa ya kidijitali kama YouTube, TikTok, Instagram, Facebook na Spotify. Majukwaa haya yamekuwa njia mbadala ya usambazaji wa kazi za sanaa, ambapo msanii anaweza kuwasiliana moja kwa moja na mashabiki wake bila kupitia kwa mawakala wa kati. Hali hii imeongeza uhuru wa kisanii, kukuza hadhira ya kimataifa na kuongeza mapato ya moja kwa moja kwa wasanii kupitia matangazo, ushirikiano wa kibiashara na mauzo ya moja kwa moja.


Zaidi ya hayo, teknolojia ya kisasa imefungua milango kwa ubunifu usio na mipaka. Wasanii sasa wanatumia programu na vifaa vya kidijitali kutengeneza muziki, video, vibonzo, sanaa za picha na kazi nyingine za ubunifu kwa ufanisi mkubwa. Hii si tu kwamba imerahisisha mchakato wa uzalishaji, pia imeongeza ubora wa kazi za sanaa. Kwa kutumia teknolojia kama Artificial Intelligence (AI), uhariri wa sauti na video wa hali ya juu, pamoja na majukwaa ya kujifunza mtandaoni, wasanii wameweza kuboresha taaluma zao, kufikia viwango vya kimataifa na kushindana katika soko la sanaa la kidunia.

Ili kujenga sanaa imara nchini, ni lazima kutambua na kuthamini mchango wa wasanii kama nguzo kuu ya maendeleo. Serikali, taasisi binafsi, vyombo vya habari na jamii kwa ujumla, vinapaswa kushirikiana na wasanii kwa kuwapa fursa za mafunzo, mitaji, masoko na mazingira rafiki ya kufanya kazi. Wasanii ni sauti ya taifa; na kupitia wao, Tanzania inaweza kujenga jamii yenye mshikamano, ubunifu na maendeleo endelevu.

Baraza la Sanaa la Taifa

**BASATA**

# JIRASIMISHE



# Daima Moyoni Mwetu



Baraza ,Uongozi na Wafanyakazi wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) wanaendelea kukukumbuka mpendwa wetu na mwenzetu, **Ndugu Japhet Mkimbila**, aliyefariki dunia mwezi Julai 2025.

Tutamkumbuka daima kwa bidii yake, unyenyekevu, na kujitolea kwake kwa dhati katika kukuza sanaa na wasanii nchini Tanzania. Mchango wake wa kazi, hekima yake, na wema wake vimeacha alama kubwa si tu ndani ya Baraza bali pia katika jamii ya wasanii kwa ujumla.

Alikuwa mtu wa uadilifu, nguzo ya mshikamano, na muumini wa kukuza vipaji. Kupitia maono na juhudi zake, aliwahamasisha wengi na kuacha urithi utakaotuongoza kwa vizazi vijavyo.

Ingawa hatupo naye kimwili tena, roho yake, mchango wake, na joto la upendo aliolitoa vitaendelea kuishi mioyoni mwetu.

Tunatoa pole za dhati kwa familia yake, ndugu, jamaa na wote waliomfahamu. Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi.

Daima katika kumbukumbu zetu,



8 Barabara ya Kivukoni,
Utumishi, Kitalu C,
S. L. P 4779,
DAR ES SALAAM.

Simu: +255 696 466 827
Baruapepe: km@basata.go.tz
info@basata.go.tz

**Mfumo wa Wadau wa Sanaa,
Jisajili kupitia: https://sanaa.go.tz**

**www.basata.go.tz**

**basata.tanzania**